Mafundisho na Maagano 101

# Fumbo la Kabaila: Fundisho katika Utiifu

Mafundishi na Maagano 101:43–62 inatoa fumbo ambalo lilitolewa kuelezea kwa nini Watakatifu walifukuzwa kutoka Missouri.

**Je, niliwahi kuhoji juu ya amri za Mungu?**
Mmewahi, kama watumushi, kuwahi kushangaa ikiwa amri ilikuwa hakika ya lazima? Fumbo hili linatufundisha kwamba amri za Bwana hutulinda na kutusaidia sisi kuishi maisha ya furaha (ona pia Mosia 2:41; Mafundisho na Maagano 82:8–10).

Je, tunaweza kufanya nini kama hatuoni uhitaji wa amri?

- Jifunze mada na usali katika Bwana kutusaidia "kuhisi kwamba ni sahihi." (Mafundisho na Maagano 9:8).
- Kumbuka nyakati katika siku za kale wakati utiifu ulipoleta baraka.[1]
- Tenda katika imani, tukiamini kwamba tutaelewa "baada ya majaribu ya imani [yetu]" (Etheri 12:6).



Katika fumbo, mtumwa anaanza kujenga mnara lakini baadae anaamua kwamba "hakuna uhitaji" kwa ajili yake (Mafundisho na Maagano 101:49). Ila kwa sababu hawajengi mnara, hawana tahadhari wakati adui atakapovunja na kuharibu shamba la mizabibu.

**Kabaila** *huagiza watumishi wake kulima shamba la mizabibu na kujenga ua kuzunguka miti na mnara ili kwamba mlinzi anaweza kuangalia juu ya nchi yote.*

**Watumishi** *hupanda shamba la mizabibu na kujenga kingo lakini wakaamua kutojenga mnara.*

**Adui asiyetarajiwa** *uharibu shamba la mzabibu.*

VIELELEZO NA BEN SIMONSEN

**MUHTASARI**
1. Ona Neil L. Andersen, "Kumbukumbu za Kuelekeza Kiroho," *Liahona,* Mei 2020, 18–22.